



THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU

THE HANSARD

Wednesday, 11th March, 2026

*The Assembly met at the
Main Chambers, at 10:30 a.m.*

[Deputy Speaker (Hon. Paul Kimani Njuguna) in the Chair]

PRAYERS

Speaker (Hon. Paul Kimani Njuguna): Next Order.

Clerk-at-the-Table: Notices of Motion

NOTICE OF MOTION

Hon. Beatrice Wamaitha Munge(Nominated): Thank you, Honorable Speaker. I beg to give notice of the following Motions:

THAT, pursuant to the provisions of the Constitution of Kenya, the County Governments Act No. 17 of 2012, and the County Assembly Standing Orders, this House adopts the Report of the Select Committee on Public Accounts on the consideration of the financial operations of the Lamu County Levy Fund for the financial year ending 30th June 2025, laid on the Table of the House on Wednesday, 4th March 2026.

Honorable Speaker. I beg to give notice of the following Motions:

THAT, pursuant to the provisions of the Constitution of Kenya, the County Governments Act No. 17 of 2012, and the County Assembly Standing Orders, this

House adopts the Report of the Select Committee on Public Accounts on the consideration of the financial operations of the County Levy Fund for the financial year ending 30th June 2025, laid on the Table of the House on Wednesday, 4th March 2026.

Honorable Speaker. I beg to give notice of the following Motions:

THAT, pursuant to the provisions of the Constitution of Kenya, the County Governments Act No. 17 of 2012, and the County Assembly Standing Orders, this House adopts the Report of the Select Committee on Public Accounts on the consideration of the financial operations of the Lamu County Emergency Fund for the financial year ending 30th June 2025, laid on the Table of the House on Wednesday, 4th March 2026.

Speaker (Hon. Paul Kimani Njuguna): Next Order.

Clerk-at-the-Table: Motion

MOTION

The County Public Investment and Accounts Committee Report on the Lamu County Disability Fund for the Year Ended 30th June 2025

Hon. Beatrice Wamaitha Munge(Nominated): Thank you, Honorable Speaker.

Honorable Speaker, I beg to move the following Motion:

THAT, pursuant to the provisions of the Constitution of Kenya, the County Governments Act No. 17 of 2012, and the County Assembly Standing Orders, this House adopts the Report of the Select Committee on Public Accounts on the consideration of the Financial Statements of the Lamu County Disability Fund for the year ended 30th June 2025, laid on the Table of the House on Wednesday, 4th March 2025.

Honorable Speaker, with your permission, I will proceed directly to highlight the key findings of the report.

I wish to confirm that the Committee comprised the following Members: Hon. Atwa, Hon. Ikris, Hon. Johnboro, Hon. Wusafu, Hon. Fahad, and Hon. Hope.

Honorable Speaker, the Committee examined the Financial Statements of the Lamu County Disability Fund for the year ended 30th June 2025, as audited by the Auditor-General.

The Auditor-General issued an opinion that the financial statements present fairly, in all material respects, the financial position of the Fund. The statements comply with the International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) – Accrual Basis, the Lamu County Persons with Disabilities Act, 2018, and the Public Finance Management Act, 2012.

However, Honorable Speaker, the audit raised concerns regarding an unresolved prior year matter.

The Committee considered the Auditor-General's observations, the responses by Management, and thereafter made the following key recommendations:

Establishment of Resource Centres

The Committee recommends the establishment of resource centres for persons living with disabilities to enhance service delivery.

Resource Mobilization

Management should mobilize additional resources from stakeholders and development partners to strengthen the Fund.

Fund Legislation

On the failure to develop comprehensive fund legislation, the Committee recommends the submission of an Amendment Bill to strengthen the implementation of the Lamu County Persons with Disabilities Act, 2018.

Honorable Speaker, that marks the summary of the report. I now request Hon. Francis to second the Motion.

Seconder

Hon. Francis Gakure Gakonga(Bahari): Asante sana, Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, ninasimama kuunga mkono hoja hii iliyowasilishwa na Kamati ya Uwekezaji na Hesabu za Umma. Ripoti hii ni muhimu sana kwani inahusu usimamizi wa Mfuko wa Walemavu katika Kaunti ya Lamu. Nawapongeza wajumbe wa kamati kwa kazi nzuri na ya kina waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, kamati imebainisha umuhimu wa kushirikisha wadau mbalimbali ili kuongeza rasilimali za mfuko huu. Hatua hii itasaidia kuhakikisha kuwa watu wanaoishi na ulemavu wanapata msaada unaostahili na huduma bora zaidi. Aidha, pendekezo la kuanzisha vituo vya rasilimali ni la msingi sana, kwani litasaidia kuboresha upatikanaji wa huduma kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kusesitiza umuhimu wa kuimarisha mfumo wa kisheria wa mfuko huu kupitia marekebisho ya sheria ili kuhakikisha usimamizi bora na uwajibikaji.

Kwa hivyo, Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na kuiomba Bunge liipitishe.

Asante sana.

Members Contribution

Hon. Amina Hassan Bwanamkuu(Nominated): Asante, Mheshimiwa Spika.

Napenda kutoa mchango wangu kuhusu suala hili. Kwanza, imebainika kuwa ni watu wachache wanaonufaika na fursa zilizopo, huku wengi wakibaki nyuma. Hali hii imeleta malalamiko miongoni mwa wananchi, hasa kuhusu ukosefu wa usawa katika ugawaji wa rasilimali na huduma.

Mheshimiwa Spika, kuna pia changamoto zinazowakumba wananchi wachache wanaojitokeza kufuatilia haki zao, ikiwemo kukosa msaada unaostahili na

kukumbana na vikwazo mbalimbali. Wengine wamekuwa wakilalamika kuwa hawapati huduma kwa wakati au wanapuuzwa wanapowasilisha hoja zao.

Kwa msingi huo, naomba Serikali ya Kaunti ichukue hatua za haraka kuhakikisha usawa, uwazi, na uwajibikaji vinaimarishwa ili wananchi wote wanufaike ipasavyo.

Hon. James Njaaga Kariuki(Hindi): Asante sana, Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii. Nami nasimama kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ripoti hii ni nzuri na yenye umuhimu mkubwa. Tukikumbuka kwamba watu wanaoishi na ulemavu siyo kwamba si watu kamili, bali ni wanajamii wenye haki sawa kama wengine. Nakumbuka maneno ya marehemu Rais Mwai Kibaki aliyesema, “Disability is not inability.”

Kwa hivyo, watu hawa bado wana umuhimu mkubwa katika jamii. Kutokuwepo kwa mfuko maalum wa kuwasaidia katika kaunti ni jambo linaloweza kutafsiriwa kama ukiukaji wa Katiba ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, nimeona pia Kamati imependekeza Serikali ya Kaunti kushirikiana na washikadau mbalimbali ili kuimarisha mfuko huu. Hili ni pendekezo muhimu sana ili kuhakikisha watu hawa wanapata msaada unaostahili.

Aidha, kuna marejeo ya Muswada wa mwaka 2018 ambao unahitaji kufuatiliwa ili kuhakikisha unatekelezwa ipasavyo. Hivyo basi, tuna jukumu kama Bunge kuhakikisha mapendekezo ya ripoti hii yanatekelezwa kikamilifu.

Ninapongeza Kamati kwa kazi nzuri, lakini pia tunapaswa kuhakikisha utekelezaji wake.

Kwa hayo machache, Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Hon. Shekhuna Abass Shekhuna(Mkomani): Asante sana, Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa aliyeleta hoja hii pamoja na Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya. Suala la watu wanaoishi na ulemavu ni la msingi sana katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, hoja hii imeletwa kwa wakati muafaka. Mara nyingi tunaona watu hawa wakikumbukwa wakati wa misaada ya chakula pekee, lakini baada ya hapo wanasahaulika. Hii si sahihi. Tunapaswa kuhakikisha wanapata msaada endelevu, si wa msimu tu.

Ni muhimu pia kutambua kuwa hakuna anayepanga kupata ulemavu; ni hali inayoweza kumpata yeyote. Hivyo basi, tunapaswa kuwa na mifumo thabiti ya kuwasaidia ndugu zetu hawa.

Naomba Kamati isiishie kutoa ripoti pekee, bali ifuatilie utekelezaji wake kikamilifu.

Kwa hayo machache, Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Hon. Beatrice Wamaitha Munge(Nominated): Thank you, Honourable Speaker. Honourable Speaker, I wish to thank all Honourable Members for their valuable contributions and for supporting this Motion. I also wish to appreciate the Committee for the good work done in bringing out these important issues.

Without much ado, Honourable Speaker, I now call upon this Honourable House to adopt the Motion.

Thank you.

Speaker (Hon. Paul Kimani Njuguna): Next Motion.

MOTION

*Adoption Of The Report Of The County Public Investment and Accounts Committee and
Approval of The Committees Consideration on The Financial Operations of The Lamu
County Youth Development Fund For The Year Ended 30th June 2025*

Hon. Beatrice Wamaitha Munge(Nominated): Thank you Honourable Speaker.

Mr. Speaker Sir, allow me to move the following motion on the floor of the House;

THAT, Pursuant to the Provision of Constitution of Kenya, County Government Act No. 17 of 2012 and the County Assembly Standing Order this House adopts the report of the Select Committee on Public Accounts and approves consideration of Lamu County Youth Development Fund for the year ended 30th June 2025. Laid on the Table of the House on Wednesday 4th March 2026.

Seconded

Hon. Francis Gakure Gakonga(Bahari): Asante sana, Mheshimiwa Spika.

Nimesimama hapa kuunga mkono ripoti ya Kamati ya Uwekezaji na Hesabu za Umma kuhusiana na matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa kifedha unaoishia tarehe 30 Juni 2025.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kuipongeza kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuchambua ripoti hii kwa kina.

Mheshimiwa Spika, ninapoendelea kuunga mkono ripoti hii, napenda kubainisha kuwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliipitia ripoti hii na kubaini matumizi kadhaa ya fedha ambayo yanazua maswali. Miongoni mwa matumizi hayo ni kiasi cha takribani shilingi milioni 3.3 kilichotumika kununua viti. Aidha, kulikuwa na matumizi mengine kwa ajili ya tamasha za muziki, tamasha za utamaduni, pamoja na utoaji wa zawadi kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihani ya shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, Mkaguzi Mkuu alieleza kuwa matumizi haya hayalingani kikamilifu na madhumuni ya mfuko huu, ambayo kimsingi ni kuwasaidia vijana

***Disclaimer:** The electronic version of the Assembly Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Office of the Clerk.*

kupitia mafunzo ya kibiashara, kuanzisha biashara, na kufuatilia maendeleo yao ili kuhakikisha wananufaika ipasavyo.

Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, wasimamizi wa mfuko huu walijitetea wakieleza kuwa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2012 inaruhusu matumizi hayo, na kwamba pia kumekuwa na marekebisho ya sheria yanayotoa mwanya huo.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ilipendekeza kuwa ni muhimu kwa wahusika kuwasilisha marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2018 ndani ya muda wa siku tisini (90), ili kuondoa mkanganyiko na kuweka mwongozo ulio wazi wa matumizi ya fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, vilevile ilibainika kuwa hakukuwa na ukaguzi wa ndani wa kutosha katika usimamizi wa mfuko huu. Ingawa wasimamizi walieleza kuwa walifanya ukaguzi wa ndani katika miaka ya 2014 na 2015, Kamati iliona kuwa ni muhimu kwa ukaguzi huo kufanywa mara kwa mara na kwa utaratibu unaoendelea.

Aidha, Mkaguzi Mkuu alibainisha ukosefu wa kanuni na taratibu zinazoweza utekelezaji mzuri wa mfuko huu. Kamati ikapendekeza kuwa wahusika waharakishe mchakato wa kuandaa na kuwasilisha kanuni hizo pamoja na marekebisho ya sheria husika ndani ya muda wa siku tisini (90).

Mheshimiwa Spika,

Kwa kuhitimisha, naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Bunge hili waunge mkono ripoti hii ili iweze kupitishwa na kusaidia kuboresha usimamizi wa fedha za vijana katika Kaunti yetu.

Asante sana, Mheshimiwa Spika.

Members' Contributions

Hon. Mathi Riziki(Nominated): Asante sana, Mheshimiwa Spika.

Nimesimama kuunga mkono ripoti ya Kamati ya Uwekezaji na Hesabu za Umma kuhusu matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa kifedha unaoishia tarehe 30 Juni 2025.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuchambua ripoti hii kwa kina.

Asante.

Mover's Response

Hon. Beatrice Wamaitha Munge(Nominated): Thank you, Honorable Speaker.

Honorable Speaker, I wish to sincerely thank all the Honorable Members for their valuable contributions to this report.

I also take this opportunity to appreciate you, Honorable Speaker, for the support and guidance you have extended to the Committee, which has enabled us to reach this final stage of consideration and adoption.

Honorable Speaker and the members in the House.

Deputy Speaker (Hon. Paul Kimani Njuguna): Next Motion.

Adoption Of The Report Of The County Public Investment and Accounts Committee and Approval of The Committees Consideration on The Financial Operations of The Lamu County Gender and Social Development Fund For The Year Ended 30th June 2025

Hon. Beatrice Wamaitha Munge(Nominated): Thank you Honourable Speaker.

Mr. Speaker Sir, allow me to move the following motion on the floor of the House;

THAT, Pursuant to the Provision of Constitution of Kenya, County Government Act No. 17 of 2012 and the County Assembly Standing Order this House adopts the report of the Select Committee on Public Accounts and approves consideration of

Lamu County Gender and Social Development Fund for the year ended 30th June 2025.

Honorable Speaker, I wish to take Members through a brief highlight of the Report. The Committee considered the Report of the Auditor-General on the Financial Statements of the Lamu County Gender and Social Development Fund for the year ended 30th June 2025.

The Committee notes that the Auditor-General expressed an unqualified opinion, stating that the financial statements present fairly, in all material respects, the financial position of the Fund as at 30th June 2025, and its financial performance and cash flows for the year then ended, in accordance with the International Public Sector Accounting Standards (IPSAS), and in compliance with the Lamu County Gender and Social Development Act, 2018 and the Public Finance Management Act, 2012.

However, Honorable Speaker, the Auditor-General raised several matters as follows:

1. Unresolved Prior Year Matters

The Auditor-General noted that some issues raised in previous audit reports remain unresolved.

The Management provided responses, and the Committee recommends that all pending issues be resolved within 90 days.

2. Irregular Expenditure / Beneficiary Compliance

The Auditor-General observed weaknesses in compliance documentation for beneficiaries.

The Committee recommends that Management ensures submission of valid KRA compliance certificates for all beneficiaries within 90 days.

3. Excessive Administrative Costs

The Auditor-General noted that administrative costs exceeded the allowable threshold. The Committee recommends that the amended Lamu County Gender and Social Development Act, 2018 be submitted within 90 days to align with Regulation 7(1)(d) of the Public Finance Management Regulations, 2015, which limits administrative costs to a maximum of 3% of the approved budget.

4. Failure to Develop Enabling Regulations

The Auditor-General observed that the Fund operates without proper enabling regulations. The Committee recommends that Management submits the necessary regulations within 90 days to ensure compliance with the law and proper governance of the Fund.

Honorable Speaker, the Committee further emphasizes the urgent need to amend the Lamu County Gender and Social Development Act, 2018 to align it with existing Public Finance Management Regulations and improve oversight of the Fund.

Honorable Speaker, that marks the end of the Committee's Report. I now call upon Honorable Francis to second. Thank you, Honorable Speaker.

Second

Hon. Francis Gakure Gakonga(Bahari): Asante sana, Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kuzungumzia kipindi hiki cha mwisho cha utekelezaji wa majukumu ya serikali ya kaunti. Katika kipindi hiki, ni muhimu kuona kwamba juhudi zinaendelea kufanywa katika kufanya marekebisho muhimu ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kuhakikisha kwamba hatua zinazochukuliwa zinaleta maendeleo ya kweli, hasa katika sekta muhimu kama vile huduma za afya, ili wananchi waweze kupata matibabu bora na kwa wakati.

Aidha, Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa idara husika kuhakikisha kwamba mipango yote iliyokusudiwa inatekelezwa ipasavyo kabla ya kipindi hiki kuhitimishwa, ili wananchi wanufaike kikamilifu na rasilimali za umma. Kwa hayo

machache, naunga mkono juhudi za kuboresha huduma na maendeleo katika kaunti yetu.

Asante, Mheshimiwa Spika.

Members' Contributions

Hon. Aisha Ali Abdulrahman(Nominated): Asante sana, Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, nami nimesimama kuunga mkono na kuchangia hoja iliyo mbele ya Bunge hili, pamoja na kuipongeza Kamati ya Uwekezaji na Hesabu za Umma kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kwanza kabisa, nawapongeza wajumbe wa kamati hiyo kwa kukaa chini, kuchunguza kwa kina, na kubaini masuala muhimu yanayoathiri utekelezaji wa shughuli katika kaunti yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Jinsia, kumekuwa na utaratibu wa kutoa fedha kwa vikundi vya wanawake, ambapo kundi lenye takriban wanachama 30 hupatiwa kiasi cha shilingi laki moja. Kwa mtazamo wangu kama mwanamke, kiasi hicho ni kidogo sana na hakiwezi kuleta mabadiliko ya maana kwa wanachama hao. Ukweli ni kwamba, fedha hizo hazitoshi kuwasaidia wanawake kuanzisha au kukuza miradi yenye tija.

Kwa hivyo, Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya kamati kwamba kuna haja ya kuongeza kiwango cha fedha kinachotolewa kwa vikundi hivi, ili kiweze kuwasaidia kwa njia ya maana – hasa katika biashara na shughuli za kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, tukilenga kuwawezesha wanawake kiuchumi, basi ni lazima tuwape rasilimali za kutosha zitakazowezesha kufikia mahitaji yao na kuboresha maisha yao.

Kwa hayo machache, naunga mkono hoja hii.

Asante, Mheshimiwa Spika.

Hon. Amina Hassan Bwanamkuu(Nominated): Asante sana, Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kuunga mkono mswada uliowasilishwa na Mheshimiwa Beatrice unaohusu Mfuko wa Jinsia.

Kwanza, Mheshimiwa Spika, imebainika kuwa kuna kiasi cha takriban shilingi milioni nne ambacho hakikuelezewa matumizi yake ipasavyo. Fedha hizi, kwa hakika, zingefaa kusaidia wananchi na kuboresha maisha yao.

Pili, Mheshimiwa Spika, imeonekana kuwa baadhi ya wanufaika hawakuorodhesha wala kuwasilisha taarifa za jinsi walivyotumia fedha walizopewa. Hii inaleta wasiwasi kuhusu uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa mfuko huu.

Kwa hivyo, Mheshimiwa Spika, naipongeza Kamati husika kwa kazi nzuri ya kung'amua masuala haya na kuyafuatilia kwa karibu.

Ninapendekeza kwamba hatua madhubuti zichukuliwe kuhakikisha kuwa nyaraka zote muhimu, ikiwemo vyeti na vielelezo vinavyohibitisha matumizi ya fedha, vinawasilishwa kwa wakati na kuhakikiwa ipasavyo.

Kwa hayo machache, naunga mkono mswada huu.

Asante sana, Mheshimiwa Spika.

Mover's Response

Hon. Beatrice Wamaitha Munge(Nominated): Thank you, Honorable Speaker.

Honorable Speaker, I wish to sincerely thank all Honorable Members who have contributed to this Motion, including those who have supported it in spirit.

I appreciate the valuable insights and commitment demonstrated by the Members during this debate.

Honorable Speaker, I now urge this House to unite and adopt this Motion, so that we can move forward in addressing the matters raised for the benefit of our wananchi.

Thank you, Honorable Speaker.

Deputy Speaker (Hon. Paul Kimani Njuguna): Next Motion.

MOTION

*Adoption of The Report Of The County Public Investment and Accounts Committee and
Approval of The Committees Consideration on The Financial Operations of The Lamu
County Bursary and Scholarship Fund For The Year Ended 30th June 2025*

Hon. Beatrice Wamaitha Munge(Nominated): Thank you Honourable Speaker.

Mr. Speaker Sir, allow me to move the following motion on the floor of the House;

THAT, Pursuant to the Provision of Constitution of Kenya, County Government Act No. 17 of 2012 and the County Assembly Standing Order this House adopts the report of the Select Committee on Public Accounts and approves consideration of Lamu County Bursary and Scholarship Fund for the year ended 30th June 2025. Laid on the Table of the House on Wednesday 4th March 2026.

Honourable Speaker, I wish to confirm that the members of the County Public Investment and Accounts Committee (CPIAC) who undertook this exercise were Honourable Atua, Honourable Bickridge, Honourable John, Honourable Husnif, Honourable Fahaad, and Honourable Hope.

Honourable Speaker, allow me to express our sincere gratitude for the support you accorded this Committee, which enabled it to effectively execute its mandate.

Honourable Speaker, as outlined on page 5 of the report, the Committee reviewed the financial statements of the Lamu County Bursary and Scholarship Fund for the year ended 30th June 2025. The Office of the Auditor-General audited these statements and issued an unqualified opinion, confirming that the financial statements present fairly, in all material respects, the financial position of the Fund as at 30th June 2025, and its financial performance and cash flows for the year then ended. This was in accordance with International Public Sector Accounting

Disclaimer: The electronic version of the Assembly Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Office of the Clerk.

Standards and in compliance with the Lamu County Bursary Fund Act, 2019, and the Public Finance Management Act.

Honourable Speaker, on the matter of resolved prior year issues, the Auditor-General had raised two key concerns:

First, the failure to develop bursary and scholarship regulations. Management reported progress, and the Committee recommended that the finalized regulations be submitted to the County Assembly for tabling.

Secondly, irregular expenditure on scholarships and other educational benefits. Management responded, and the Committee resolved to keep the matter under review.

Honourable Speaker, the Committee further considered several audit queries and made the following recommendations:

On the failure to develop bursary and scholarship regulations, the Committee reiterated its recommendation for their submission to the County Assembly.

On the incomplete composition of the Fund Board, the Committee noted the Auditor-General's observations and management's response, and recommended that the CECM for Education urgently submit two new nominees to replace those previously rejected. Honourable Speaker, I wish to emphasize that this recommendation was a firm directive, and the Committee expects immediate compliance upon adoption of this Motion.

On the issue of irregular award of bursaries, the Committee recommended submission of the ward bursary committee list as required.

On the failure to acknowledge receipt of bursary and scholarship awards, the Committee recommended that school heads submit acknowledgement letters together with schedules of original receipts to the bursary office.

On payments made outside the mandate of the County Government, the Committee noted that the matter is under intergovernmental deliberations and resolved to keep it under review.

Honourable Speaker, Honourable Members, I now urge this House to adopt this Report. Thank you, Honourable Speaker.

At this juncture, I call upon Honourable Francis to second the Motion.

Second

Hon. Francis Gakonga(Nominated): Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu kuhusu ripoti ya matumizi ya fedha za basari na pia fedha za utafiti wa masomo.

Mheshimiwa Spika, ripoti hii ni nzuri na inaonyesha kuwa ukaguzi ulifanyika kwa kina kuhusu matumizi ya fedha hizi ndani ya kaunti na kwa kuzingatia mifumo ya kitaifa. Kamati ilifanya kazi yake kwa ustadi, na tunapaswa kuipongeza kwa juhudi hizo. Pia, tunatambua kuwa wakati wa ukaguzi, wahusika kutoka idara husika waliitwa na walitoa ushirikiano wao.

Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, ripoti imebaini mapungufu kadhaa. Kwanza, imeelezwa kuwa fedha za basari hazina kanuni madhubuti za kuzisimamia. Ingawa wahusika walieleza kuwa kanuni hizo tayari zimeandaliwa, bado hazijawasilishwa mbele ya Bunge hili ili ziweze kujadiliwa na kupitishwa. Hivyo basi, kamati inapendekeza kuwa kanuni hizo ziwasilishwe haraka iwezekanavyo ili Bunge liweze kuzithibitisha.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala la matumizi ya fedha hizi katika maeneo ambayo si ya mamlaka ya kaunti. Mkaguzi alieleza kuwa baadhi ya shughuli zilizofadhiliwa zinapaswa kufanywa na serikali kuu, hasa kupitia Wizara ya Elimu. Hata hivyo, wasimamizi wa fedha hizi walieleza kuwa kuna makubaliano yanayoendelea kati ya kaunti na Wizara ya Elimu ili kuhalalisha matumizi hayo. Ni muhimu basi makubaliano hayo yawekwe wazi na kuwasilishwa rasmi.

Aidha, Mheshimiwa Spika, wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa bodi inayosimamia fedha hizi haikuwa na idadi kamili ya wanachama, ikiwa na watu sita badala ya tisa kama inavyotakiwa. Hali hii inaathiri ufanisi na uwajibikaji wa bodi hiyo. Ni vyema majina ya wanachama waliobaki yawasilishwe kwa Bunge hili ili yaidhinishwe bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na upungufu katika uwakilishi ndani ya bodi hiyo. Mkaguzi hakupata ushahidi wa uwepo wa mwakilishi wa vijana na pia mwakilishi wa watu wanaoishi na ulemavu, jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya kisheria na usawa wa kijamii. Hii ni kasoro inayopaswa kurekebishwa mara moja.

Kwa kumalizia, Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Bunge hili kuunga mkono ripoti hii ili mapendekezo yake yaweze kutekelezwa na kuboresha usimamizi wa fedha hizi muhimu kwa wananchi wetu.

Asante sana, Mheshimiwa Spika.

Members' Contribution

Hon. James Njaaga Kariuki(Hindi): Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi tena ili niweze kusimama na kuunga mkono mswada ulioko mbele yetu.

Kwanza, napenda kuishukuru kamati husika kwa kuwasilisha ripoti iliyoandaliwa kwa mtiririko mzuri na kwa umakini. Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia ripoti hii kwa kina, nimebaini kuwepo kwa mapungufu kadhaa ambayo yanahitaji kushughulikiwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya mapungufu hayo ni kutokuwepo kwa kamati za bursary katika baadhi ya wodi, hususan Wodi ya Witu na Wodi ya Basuba. Hali hii inaleta mashaka kuhusu nani anahusika katika mchakato wa kuchagua wanufaika wa bursary, na iwapo haki inatendeka kwa wanafunzi wote wanaostahili.

Aidha, Mheshimiwa Spika, ripoti inaonyesha kuwa ingawa fedha za bursary zinatolewa, kuna changamoto katika uthibitishaji wa kufika kwa fedha hizo mashuleni. Risiti na nyaraka za kuthibitisha kupokelewa kwa fedha hizo haziko

Disclaimer: The electronic version of the Assembly Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Office of the Clerk.

wazi au hazijakamilika ipasavyo. Hii inaleta wasiwasi kuhusu uwajibikaji na ufuatiliaji wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, suala la usimamizi wa fedha, hasa katika kaunti yetu, linahitaji umakini wa hali ya juu. Bila mifumo thabiti, kuna hatari ya kuwepo kwa wanafunzi hewa (ghost beneficiaries) wanaonufaika na fedha hizi bila kustahili. Ndiyo maana kamati ilisisitiza umuhimu wa kuunda kamati za bursary katika kila wodi ili kuhakikisha kuwa wanaonufaika ni watoto halali wa kaunti hii.

Kwa hivyo, Mheshimiwa Spika, nawapongeza wanakamati kwa kazi nzuri waliyoifanya, lakini pia nawatahadharisha kuwa tusilegeze kamba. Mapungufu yaliyobainika ni mengi na yanahitaji hatua za haraka na za dhati.

Ningependa pia kusesitiza kuwa, kama Kamati ya Utekelezaji (Implementation Committee), tutafuatilia kwa karibu utekelezaji wa mapendekezo yote yaliyotolewa. Ndani ya kipindi cha siku 90, kama ilivyopendekezwa, tunatarajia kupata mrejesho kamili. Endapo hilo halitafanyika, basi tutawaita wahusika tena mbele ya kamati kutoa maelezo ya kina kuhusu sababu za kutotekeleza maelekezo hayo.

Kwa hayo machache, Mheshimiwa Spika, naunga mkono mswada huu, na naomba sasa wahusika waitwe kutoa majibu yao.

Asante sana, Mheshimiwa Spika.

Mover's Response

Hon. Beatrice Wamaitha Munge(Nominated): Thank you, Honourable Speaker. I wish to thank the Honourable Chairperson of the Implementation Committee for the valuable contributions he made.

Honourable Speaker, it gives us great confidence that through this collaboration, we shall be able to deliver more effective and impactful services to the people of Lamu.

To the committee and all Honourable Members present, I extend my sincere appreciation for your contributions and patience throughout the consideration of this motion. Your input has been instrumental in shaping this outcome.

Honourable Speaker, I also wish to express my gratitude to you and the Office of the Clerk for the continuous support accorded to this committee. Your guidance and facilitation have enabled us to effectively discharge our mandate in service to the citizens of Lamu.

Without much further ado, Honourable Speaker, I now urge all Members of this Honourable House to join hands and adopt this motion.

Thank you, Honourable Speaker.

(Questions put and Agreed Upon)

Speaker (Hon. Paul Njuguna Kimani): Honorable Members, there being no other business, the Assembly stands adjourned until today Wednesday, 11th March 2026 at 2:30 pm.

The Assembly rose at 12:30p.m.